

Gen

Chapter 26

Swahili Interlinear

Reference: Swahili Biblica Neno

בִּימֵי	הָיָה	אֲשֶׁר	הָרִאשׁוֹן	הָרֵעַב	מִלְבָּר	בְּאֶרֶץ	רָעַב	וַיְהִי	1
katika-siku-za	ilikuwa	ambayo	ya-kwanza	njaa	mbali-na	katika-nchi	njaa	Na-ikawa	
H3117	H1961		H7223	H7458	H0905	H0776	H7458	H1961	
	גֵּרָרָה:	פְּלִשְׁתִּים	מַלְךְ-	אֲבִימֶלֶךְ	אֶל-	יִצְחָק	וַיֵּלֶךְ	אֲבְרָהָם	
	Gerari	Wafilisti	mfalme-wa	Abimeleki	kwa	Isaka	na-akaenda	Ibrahimu	
	H1642	H6430	H4428	H0040	H0413	H3327	H3212	H0085	

Basi njaa kubwa ikawa katika nchi hiyo, kuliko ile njaa iliyotangulia iliyotokea wakati wa Abrahamu. Isaki akamwendea Abimeleki mfalme wa Wafilisti huko Gerari.

בְּאֶרֶץ	שָׁכַן	מִצְרַיִם	תָּרַד	אֶל-	וַיֹּאמֶר	יְהוָה	אֵלָיו	וַיֵּרָא	2
katika-nchi	kaa	Misri	shuke	usi	na-akasema	Yahwe	kwake	Na-akamtokea	
H0776	H7931	H4714	H3381	H0408	H0559	H3068	H0413	H7200	
						אֵלָיו:	אָמַר	אֲשֶׁר	
						kwako	nitakuambia	ambayo	
						H0413	H0559		

Bwana akamtokea Isaki, akamwambia, "Usiende Misri, bali ukae katika nchi nitakayokuambia.

כִּי-	וַאֲבָרְכֶךָ	עִמָּךְ	וַאֲהִיָּה	הִזֵּאת	בְּאֶרֶץ	גֵּוֶר	3	
kwa-sababu	na-nitakubariki	pamoja-nawe	na-nitakuwa	hii	katika-nchi	kaa-kama-mgeni		
	H1288		H1961	H2063	H0776			
וַהֲקַמְתִּי	הָאֵל	הָאֲרֶצֶת	כָּל-	אֶת-	אֶתְּךָ	וַיֵּלְצֶנּוּ	לְךָ	
na-nitaisimamisha	hizi	nchi	nchi-zote	[alama]	nitaitoa	na-kwa-uzao-wako	kwako	
	H0411	H0776	H3605	H0853	H5414	H2233		
		אָבִיךָ:	לְאֲבְרָהָם	נִשְׁבַּעְתִּי	אֲשֶׁר	הַשְּׂבֻעָה	אֶת-	
		baba-yako	kwa-Ibrahimu	niliapa	ambacho	kiapo	[alama]	
		H0001	H0085	H7650		H7621	H0853	

Kaa katika nchi hii kwa kitambo, mimi nitakuwa pamoja na wewe na nitakubariki. Kwa maana nitakupua wewe na uzao wako nchi hizi zote na nitatimiza kiapo nilichomwapia Abrahamu baba yako.

לְזַרְעֶךָ	וַנִּיתֵי	הַשָּׁמַיִם	כְּכּוֹכְבֵי	זַרְעֶךָ	אֶת-	וַהֲרַבִּיתִי	4	
kwa-uzao-wako	na-nitaitoa	za-mbinguni	kama-nyota	uzao-wako	[alama]	Na-nitazidisha		
H2233	H5414	H8064	H3556	H2233	H0853			
גּוֹיֵי	כָּל	בְּזַרְעֶךָ	וַהֲתַבְּרִכּוּ	הָאֵל	הָאֲרֶצֶת	כָּל-	אֶת	
ya-mataifa	mataifa-yote	katika-uzao-wako	na-watajibariki	hizi	nchi	nchi-zote	[alama]	
	H3605	H2233	H1288	H0411	H0776	H3605	H0853	
						הָאֲרֶץ:		
						ya-dunia		
						H0776		

Nitafanya wazao wako kuwa wengi kama nyota za angani, nami nitawapa nchi hizi zote na kutokana na uzao wako mataifa yote yatabarikiwa,

מְשֻׁמְרֵי מְשֻׁמְרֵי וַיִּשְׁמֵר בְּקִלִּי אִבְרָהִם שָׁמַע אֲשֶׁר- לְעֵקֶב 5
 amri-yangu na-akashika sauti-yangu Ibrahimu aliisikia kwamba kwa-sababu
[H4931](#) [H8104](#) [H0085](#) [H8085](#) [H6118](#)

וְתוֹרָתִי וְתוֹרָתִי חֻקֹּתַי מִצְוֹתַי
 na-mafundisho-yangu sheria-zangu maagizo-yangu
[H8451](#) [H2708](#) [H4687](#)

kwa sababu Abrahamu alinitii mimi akatunza kanuni zangu na maagizo yangu, amri zangu pamoja na sheria zangu.”

וַיֵּשֶׁב וַיֵּשֶׁב יִצְחָק בְּגֵרָרִי :
 Na-akakaa Isaka katika-Gerari
[H3427](#) [H3327](#) [H1642](#)

Hivyo Isaki akaishi huko Gerari.

הוּא אָחֹתִי וַיֹּאמֶר לְאִשְׁתּוֹ הַמָּקוֹם אֲנִשִּׁי וַיִּשְׁאַלּוּ
 yeye dada-yangu na-akasema kuhusu-mke-wake mahali watu-wa Na-wakauliza
[H1931](#) [H0269](#) [H0559](#) [H0802](#) [H4725](#) [H0376](#) [H7592](#)

עַל- קִי יָרָא לְאִמְרָה אֲשֶׁר־ לַחֲנִי וְהָרַנִּי אֲנִשִּׁי הַמָּקוֹם
 kwa-sababu-ya mahali watu-wa wataniua labda mke-wangu kusema aliogopa kwa-sababu
[H4725](#) [H0376](#) [H2026](#) [H6435](#) [H0802](#) [H0559](#) [H3372](#)

רֵבֶקָה קִי- טוֹבַת מְרָאָה הִיא :
 Rebeka kwa-sababu mzuri wa-kuonekana yeye
[H7259](#) [H1931](#) [H4758](#)

Watu wa mahali pale walipomuuliza habari za mke wake, akasema, “Huyu ni dada yangu,” kwa sababu aliogopa kusema, “Huyu ni mke wangu.” Alifikiri, “Watu wa mahali pale wataweza kumuua kwa sababu ya Rebeka, kwa kuwa alikuwa mzuri wa sura.”

וַיְהִי וַיְהִי כִי אָרְכוּ- לֹו שָׁם הַיָּמִים וַיִּשְׁקֶף אַבִּימֶלֶךְ
 Na-ikawa wakati zilipokuwa-ndefu kwake huko siku na-akatazama-nje Abimeleki
[H1961](#) [H0748](#) [H8033](#) [H3117](#) [H8259](#) [H0040](#)

אֵת מֶלֶךְ פְּלִשְׁתִּים בְּעַד הַחֲלוֹן וַיִּרָא וְהָנָה יִצְחָק מִצְחָק הוּא
 mfalme wa-Wafilisti kupitia dirisha na-akaona na-tazama Isaka akimburudisha pamoja-na
[H4428](#) [H6430](#) [H1157](#) [H2474](#) [H7200](#) [H2009](#) [H3327](#) [H6711](#) [H0854](#)

רֵבֶקָה אֲשֶׁתּוֹ :
 Rebeka mke-wake
[H7259](#) [H0802](#)

Wakati Isaki alipokuwa amekaa huko siku nyingi, Abimeleki mfalme wa Wafilisti akachungulia dirishani, akaona jinsi Isaki alivyomkumbatia Rebeka mke wake.

וַיִּקְרָא וַיִּקְרָא אַבִּימֶלֶךְ לְיִצְחָק וַיֹּאמֶר אֵד וְהָנָה אֲשֶׁר־ הוּא וַיִּפֶּן
 Na-akamwita Abimeleki kwa-Isaka na-akasema hakika tazama mke-wako yeye na-vipi
[H7121](#) [H0040](#) [H3327](#) [H0559](#) [H0389](#) [H2009](#) [H0802](#) [H1931](#)

אֲמֹתָ אֲמֹתָ אֲחֹתִי הוּא וַיֹּאמֶר אֵלָיו יִצְחָק כִּי אֲמַרְתִּי פֶן-
 ulisema dada-yangu yeye na-akasema kwake Isaka kwa-sababu nilisema labda nitakufa
[H0559](#) [H0269](#) [H1931](#) [H0559](#) [H0413](#) [H3327](#) [H6435](#) [H0559](#) [H4191](#)

עָלֶיהָ :
 kwa-sababu-yake

Abimeleki akamwita Isaki akamwambia, “Hakika huyu ni mke wako! Mbona uliniambia, ‘Huyu ni dada yangu?’” Isaki akamjibu, “Kwa sababu nilifikiri ningeweza kuuawa kwa sababu yake.”

10
הָעַם אַחַד שָׁכַב כְּמַעַט לָנוּ עָשִׂיתָ זֹאת מַה- אַבִּימֶלֶךְ וַיֹּאמֶר
wa-watu mmoja angelala labda kwetu umefanya hiki nini Abimeleki Na-akasema
[H0259](#) [H7901](#) [H4592](#) [H2063](#) [H4100](#) [H0040](#) [H0559](#)

אַתָּה אֲשֶׁרְךָ וְהִבַּאתָ עָלֵינוּ אֵשׁ: אַתָּה
pamoja-na mke-wako na-ungeleta juu-yetu hatia
[H0817](#) [H0935](#) [H0802](#) [H0854](#)

Ndipo Abimeleki akamjibu, “Ni nini hiki ulichotufanyia? Ingewezekana mtu yeyote akawa amekutana kimwili na mke wako, nawe ungeleta hatia juu yetu.”

11
הַזֶּה בָּאִישׁ הַנֶּעַע לְאָמַר הָעַם כָּל- אֶת- אַבִּימֶלֶךְ וַיֹּצִי
huyu mtu anayemgusa akisema watu watu-wote [alama] Abimeleki Na-akaamuru
[H2088](#) [H0376](#) [H5060](#) [H0559](#) [H3605](#) [H0853](#) [H0040](#) [H6680](#)

וּבְאֵשׁוֹ מוֹת יוֹמָת: וּבְרַכְתִּי
au-mke-wake kufa atauawa
[H4191](#) [H4191](#) [H0802](#)

Hivyo Abimeleki akatoa amri kwa watu wote, akisema, “Yeyote atakayemnyanyasa : mtu huyu au mkewe hakika atauawa.”

12
שְׁעָרַיִם מָאָה הַהוּא בַשָּׁנָה לְאָמַר הָעַם וַיִּמְצָא הַהוּא בְּאֶרֶץ יִצְחָק וַיִּזְרַע
vipimo mara-mia ule katika-mwaka na-akapata ile katika-nchi Isaka Na-akapanda
[H8180](#) [H3967](#) [H1931](#) [H8141](#) [H4672](#) [H1931](#) [H0776](#) [H3327](#) [H2232](#)

יְהוָה: וּבְרַכְתִּי
Yahwe na-akambariki
[H3068](#) [H1288](#)

Isaki akapanda mazao katika nchi hiyo, kwa mwaka huo huo, akavuna mara mia, kwa sababu Bwana alimbariki.

13
כִּי- עַד וַיְגַדֵּל וַיִּגְדַּל הַלּוֹךְ וַיִּגְדַּל הָאִישׁ וַיִּגְדַּל
kwamba mpaka na-kuwa-mkubwa kuendelea na-akaendelea mtu Na-akawa-mkubwa
[H5704](#) [H1432](#) [H1980](#) [H3212](#) [H0376](#) [H1431](#)

מָאָד: נָדַל
sana akawa-mkubwa
[H3966](#) [H1431](#)

Isaki akawa tajiri, mali zake zikaendelea kuongezeka mpaka akawa tajiri sana.

14
רַבָּה וַעֲבָדָה בְּקָר וַיִּמְקְנֶה צֹאן וַיִּקְנֶה לוֹ וַיְהִי-
wengi na-watumishi ng'ombe na-makundi-ya kondoo makundi-ya kwake Na-alikuwa-na
[H5657](#) [H1241](#) [H4735](#) [H6629](#) [H4735](#) [H1961](#)

וַיִּקְנֶה: אֶתּוֹ פְּלִשְׁתִּים: וַיִּקְנֶה
na-wakamwonea-wivu yeye Wafilisti
[H6430](#) [H0853](#) [H7065](#)

Akawa na mifugo ya kondoo na ng'ombe, na watumishi wengi sana, kiasi kwamba Wafilisti wakamwonea wivu.

15
בֵּימֵי אָבִיו עַבְדֵי חֶפְרוֹ אֲשֶׁר הִבְאֵרְתָּ וְכָל-
katika-siku-za baba-yake watumishi-wa walichimba ambavyo visima Na-visima-vyote
[H3117](#) [H0001](#) [H5650](#) [H2658](#) [H0875](#) [H3605](#)

אֲבְרָהָם אָבִיו סְתָמוֹם פְּלִשְׁתִּים וַיִּמְלְאוּם עֶפְרוֹ:
Ibrahimu baba-yake waliziba Wafilisti na-wakavijaza udongo
[H6083](#) [H4390](#) [H6430](#) [H0001](#) [H0085](#)

Kwa hiyo visima vyote vilivyochimbwa na watumishi wakati wa Abrahamu baba yake, Wafilisti wakavifukia, wakavijaza udongo.

16 עֲצֻמַתּוֹ umekuwa-na-nguvu כִּי- kwa-sababu מִכְּעֻמְנוֹ kutoka-kwetu לָךְ nenda יִצְחָק Isaka אֶל- kwa אַבִּימֶלֶךְ Abimeleki וַיֹּאמֶר Na-akasema H3212 H3327 H0413 H0040 H0559

מִמְּנוּ מֵאֵד : sana kuliko-sisi H3966

Ndipo Abimeleki akamwambia Isaki, "Ondoka kwetu, kwa maana umetuzidi nguvu sana."

17 וַיֵּשֶׁב na-akakaa נָגֶרֶר Gerari בְּנִחְלַיִם katika-bonde-la וַיִּחַן na-akapiga-hema יִצְחָק Isaka מִשָּׁם kutoka-huko וַיֵּלֶךְ Na-akaondoka H3427 H1642 H2583 H3327 H8033 H3212

שָׁם : huko H8033

Basi Isaki akatoka huko akajenga kambi katika Bonde la Gerari, akaishi huko.

18 וַיֵּשֶׁב Na-akarudi יִצְחָק Isaka וַיִּנְחָר na-akachimba אֶת- [alama] בְּאֶרֶת visima הַמַּיִם vya-maji אֲשֶׁר ambavyo חֲפָרוֹ walichimba H2658 H4325 H0875 H0853 H2658 H3327 H7725

אֲבְרָהָם cha-Ibrahimu מוֹת kifo אַחֲרָיִם baada-ya פְּלִשְׁתִּים Wafilisti וַיִּסְתָּמוּם na-waliziba אָבִיו baba-yake אֲבְרָהָם Ibrahimu בֵּימֵי katika-siku-za H0085 H4194 H6430 H0001 H0085 H3117

וַיִּקְרָא na-akayaita לָהֶן kwayo שְׁמוֹת majina כְּשִׁמֹּת kama-majina אֲשֶׁר- ambayo קָרָא aliita לָהֶן kwayo אָבִיו : baba-yake H0001 H7121 H8034 H8034 H7121

Ndipo Isaki akavichimbua tena vile visima vya maji ambavyo vilichimbwa siku zile za Abrahamu baba yake, ambavyo Wafilisti walivifukia baada ya kufa Abrahamu, akavipa majina yale yale ambayo baba yake alikuwa amevipa.

19 מַיִם cha-maji בָּאֵר kisima שָׁם huko וַיִּמְצְאוּ- na-wakapata בְּנִחְלַיִם katika-bonde יִצְחָק Isaka עֲבָדָיו watumishi-wa וַיִּנְחָרוּ Na-wakachimba H4325 H0875 H8033 H4672 H3327 H5650 H2658

תַּיִם : yanayobubujika

Watumishi wa Isaki wakachimba katika lile bonde wakagundua huko kisima chenye maji safi.

20 לָנוּ ni-yetu לְאִמְרֵי wakisema יִצְחָק Isaka רָעִי wachunga-wa עִם- pamoja-na נָגֶרֶר Gerari רָעִי wachunga-wa וַיִּיבֹּנוּ Na-wakashindana H0559 H3327 H7473 H1642 H7473 H7378

הַמַּיִם maji וַיִּקְרָא na-akakiita שֵׁם- jina-la הַבָּאֵר kisima עֵשֶׂק Eseki הִתְעַשְׂקוּ walishindana כִּי kwa-sababu עָמוּ : naye H6229 H6230 H0875 H8034 H7121 H4325

Lakini wachungaji wa Gerari wakagombana na wachungaji wa Isaki wakisema, "Maji haya ni yetu!" Ndipo akakiita kile kisima Eseki, kwa sababu waligombana naye.

שָׁמָּה	וַיִּקְרָא	עָלֶיהָ	גַּם־	וַיִּרְיֶבּוּ	אֲחֵרֶת	כִּסִּימָה	וַיִּחְפְּרוּ	21
jina-lake	na-akakiita	juu-yake	pia	na-wakashindana	kingine	kisima	Na-wakachimba	
H8034	H7121		H1571	H7378	H0312	H0875	H2658	

שִׁטְנָה:
Sitna
[H7856](#)

Kisha wakachimba kisima kingine, lakini hata hicho pia wakakigombania, akakiita Sitna.

רְבוּ	וְלֹא	אֲחֵרֶת	כִּסִּימָה	וַיִּחְפְּרוּ	מִשָּׁם	וַיֵּתֶק	22
hawakushindana	na-hawa	kingine	kisima	na-akachimba	kutoka-huko	Na-akaondoka	
H7378	H3808	H0312	H0875	H2658	H8033	H6275	

הִרְחִיב	עָתָּה	כִּי־	וַיֹּאמֶר	רְחֹבֹת	שָׁמָּה	וַיִּקְרָא	עָלֶיהָ
ametufanyia-nafasi	sasa	kwa-sababu	na-akasema	Rehobothi	jina-lake	na-akakiita	juu-yake
H7337	H6258		H0559	H7344	H8034	H7121	

וַיְהִי
Yahwe
[H3068](#)

לְבוֹ
kwetu

וּפְרִינוּ
na-tutazaa
[H6509](#)

בְּאֶרֶץ:
katika-nchi
[H0776](#)

Akaondoka huko, akachimba kisima kingine, wala hakuna yeyote aliyekigombania. Akakiita Rehobothi, akisema, "Sasa Bwana ametufanyia nafasi, nasi tutastawi katika nchi."

וַיֵּעַל	מִשָּׁם	שֶׁבַע־בְּעָרַיִם	23
Na-akapanda	kutoka-huko	Beer-Sheba	
H5927	H8033	H0884	

Kutoka pale akaenda Beer-Sheba.

אֲבְרָהָם	אֱלֹהֵי	אִמִּי	וַיֹּאמֶר	הָהוּא	בְּלַיְלָה	יְהוָה	אֵלָיו	וַיָּרָא	24
Ibrahimu	Mungu-wa	Mimi	na-akasema	ule	usiku	Yahwe	kwake	Na-akamtokea	
H0085	H0430	H0595	H0559	H1931	H3915	H3068	H0413	H7200	

וַהֲרִבֵּיתִי	וַיִּבְרַכְתִּיךָ	אִמִּי	אֶתְּךָ	כִּי־	תִּירָא	אֶל־	אֲבִיךָ
na-nitazidisha	na-nitakubariki	Mimi	pamoja-nawe	kwa-sababu	ogope	usi	baba-yako
	H1288	H0595	H0854		H3372	H0408	H0001

אֶת־
[alama] [H0853](#)

זֶרְעֶךָ
uzao-wako [H2233](#)

בְּעֵבֶר
kwa-ajili-ya [H5668](#)

אֲבְרָהָם
Ibrahimu [H0085](#)

עֲבָדִי:
mtumishi-wangu [H5650](#)

Usiku ule Bwana akamtokea, akamwambia, "Mimi ndimi Mungu wa Abrahamu baba yako. Usiogope, kwa maana mimi niko pamoja nawe, nitakubariki na kuongeza idadi ya wazao wako kwa ajili ya Abrahamu mtumishi wangu."

אֶהְלֶה	שָׁם	וַיִּטֵּ־	יְהוָה	בְּשֵׁם	וַיִּקְרָא	מִזְבֵּחַ	שָׁם	וַיִּבֶן	25
hema-lake	huko	na-akapiga	la-Yahwe	kwa-jina	na-akaita	madhabahu	huko	Na-akajenga	
H0168	H8033	H5186	H3068	H8034	H7121	H4196	H8033	H1129	

וַיִּכְרוֹ־
na-wakachimba

שָׁם
huko [H8033](#)

עֲבָדֵי־
watumishi-wa [H5650](#)

יִצְחָק
Isaka [H3327](#)

כִּסִּימָה:
kisima [H0875](#)

Isaki akajenga madhabahu huko, akaliitia jina la Bwana. Akapiga hema lake huko, nao watumishi wake wakachimba kisima.

26 שר- mkuu-wa H8269 ופיקל na-Fikoli H6369 מרעהו rafiki-yake H4828 ואחזת na-Ahuzathi H0276 מנרר kutoka-Gerari H1642 אליו kwake H0413 הלך akaenda H1980 ואבימלקי Na-Abimeleki H0040

צבאו :
jeshi-lake

Wakati huo, Abimeleki alikuwa amemjia kutoka Gerari, akifuatana na Ahuzathi mshauri wake, pamoja na Fikoli jemadari wa majeshi yake.

27 אתי mimi H0853 שנאתם mlinichukia H8130 ואתם na-ninyi ואליו kwangu H0413 באתם mmekuja H0935 מדוע kwa-nini H4069 יצחק Isaka H3327 אלהם kwao H0413 ויאמר Na-akasema H0559

ותשלחני na-mkanituma H7971
מאתכם :
kutoka-kwenu H0854

Isaki akawauliza, “Mbona mmekuja kwangu na ninyi mlinichukia na kunifukuza?”

28 ויאמר na-tukasema H0559 עמך pamoja-nawe ויהוה Yahwe H3068 היה amekuwa H1961 כי- kwamba ראינו tumeona H7200 ראו tumeona H7200 ויאמרו Na-wakasema H0559

תהי iwe H1961 נא tafadhali H4994 אלה kiapo H0423 בינותינו kati-yetu H0996 בינינו kati-yetu H0996 ובינך na-kati-yako H0996 ונכרתה na-tufanye H3772 ברית agano H1285 עמך : pamoja-nawe

Wakamjibu, “Tuliona wazi kuwa Bwana alikuwa pamoja nawe, kwa hiyo tukasema, ‘Inabidi kuwe na kiapo cha mapatano kati yetu, kati yetu na wewe. Na tufanye mkataba pamoja nawe

29 עשיתי tulivyofanya H5060 וכאשר na-kama H5060 נגעננו kukugusa H3808 לא hatuku כאשר kama רעה ubaya עמנו kwetu תעשה kufanya אם- kwamba-huta

עמך kwako H7535 רק- tu H7535 טוב wema ונשלחך na-tukakuondoa H7971 בשלום kwa-amani H7965 אתה wewe עתה sasa H6258 ברוך mbarikiwa H1288 יהוה : wa-Yahwe H3068

kwamba hutatudhuru, kama jinsi nasi hatukuwanyanyasa bali tuliwatendea mema wakati wote na kuwaondoa kwetu kwa amani. Tena sasa umebarikiwa na Bwana.”

30 וישאו na-wakanywa H8354 ויאכלו na-wakala H0398 משנה karamu H4960 להם kwao ויעש Na-akawafanyia

Basi Isaki akawaandalia karamu, nao wakala na kunywa.

31 וישלחם na-akawaondoa H7971 לאחיו kwa-ndugu-yake H0251 איש mtu H0376 וישבעו na-wakaapiana H7650 בכך asubuhi H1242 וישכימו Na-wakaamka-mapema H7925

יצחק Isaka H3327 וילכו na-wakaenda H3212 מאתו kutoka-kwake H0854 בשלום : kwa-amani H7965

Kesho yake asubuhi na mapema, wakaapizana wao kwa wao. Kisha Isaki akawaruhusu waende zao, wakamwacha Isaki kwa amani.

לֹו	וַיִּגְדֹו	יִצְחָק	עֲבָדֵי	וַיָּבֹאוּ	הָהוּא	בֵּינִים	וַיְהִי	32
kwake	na-wakamwambia	Isaka	watumishi-wa	na-wakaja	ile	katika-siku	Na-ikawa	
	H5046	H3327	H5650	H0935	H1931	H3117	H1961	

מַיִם:	מְצֹאנוּ	לֹו	וַיֹּאמְרוּ	חֲפְרוּ	אֲשֶׁר	חֲבָאָר	אֲדוֹת	עַל-
maji	tumepata	kwake	na-wakasema	walichimba	ambacho	kisima	habari-za	kuhusu
H4325	H4672		H0559	H2658		H0875	H0182	

Siku hiyo watumishi wa Isaki wakaja wakampa habari kuhusu kisima walichokuwa wamekichimba, wakamwambia, "Tumepata maji!"

הַיּוֹם	עַד	שֶׁבַעבְּאָר	הָעִיר	שֵׁם-	כֵּן	עַל-	שֶׁבַעַה	אֶחָה	וַיִּקְרָא	33
siku	hadi	Beer-Sheba	mji	jina-la	hivyo	kwa-sababu-ya	Shiba	hicho	Na-akakiita	
H3117	H5704	H0884		H8034			H7656	H0853	H7121	

ס	הַזֶּה:
[sehemu]	hii
	H2088

Naye akakiita Shiba, mpaka leo mji huo unaitwa Beer-Sheba.

אֶת-	אִשָּׁה	וַיִּקַּח	שָׁנָה	אַרְבָּעִים	בֶּן-	עֵשָׂו	וַיְהִי	34
[alama]	mke	na-akamchukua	miaka	arobaini	mwenye-miaka	Esau	Na-Esau-alikuwa	
H0853	H0802	H3947	H8141	H0705		H6215	H1961	

קַחְתִּי:	אֵילֹן	בַּת-	בְּשֵׁמֶת	וְאֶת-	קַחְתִּי	בְּאָרֵי	בַּת-	יְהוּדִית
Mhiti	Eloni	binti-ya	Basemathi	na-pia	Mhiti	Beeri	binti-ya	Yudithi
H2850	H0356	H1323	H1315	H0853	H2850	H0882	H1323	H3067

Esau alipokuwa na umri wa miaka arobaini, akamwoa Yudithi binti Beeri Mhiti, kisha akamwoa Basemathi binti Eloni Mhiti.

ס	וַלְרֵבֶקָה:	לְיִצְחָק	רוּחַ	מִרְתַּ	וַתְהַיָּו	35
[sehemu]	na-kwa-Rebeka	kwa-Isaka	wa-roho	uchungu	Na-walikuwa	
	H7259	H3327	H7307	H4786	H1961	

Hawa walikuwa chanzo cha huzuni ya Isaki na Rebeka.